

KUNYAKULIWA

Kwa sababu Bwana mwenyewe atashuka kutoka Mbinguni pamoja na mwaliko, na sauti ya malaika Mkuu, na parapanda ya Mungu; nao waliokufa katika Kristo watafufuliwa kwanza. Kisha sisi tulio hai, tulio salia, tutanyakuliwa pamoja nao katika mawingu, ili tu mlaki Bwana hewani; na hivyo tutakuwa pamoja na Bwana milele (1 Wathesalonike 4:13-18).

Sikiliza kile Nabii wa Mungu alichosema juu ya hilo:

Lakini kwa kanisa yule Bibi Arusi, kunyakuliwa ni Ufunuo kwake. Imefunuliwa kwake. Kuwa ufunuo huo, yule Bibi Arusi wa kweli wa Kristo atakuwa akingoja ufunuo huo wa kunyakuliwa sasa, ni ufunuo, kuwa na ufunuo ni Imani (Waebrania 11:1). Huwezi kuwa na ufunuo bila huo ufunuo kuwa ni Imani. Imani ni ufunuo kwa sababu ni kitu fulani kimefunuliwa kwako. Imani ni ufunuo, **Imani ni kitu fulani kilichofunuliwa kwako kama ilivyo kuwa kwa Ibrahim. Ambacho kingetaja kitu chochote kinyume cha yale yaliokuwa yamefunuliwa kwake kana kwamba hakikuwapo (Warumi 4:13-21).** Hivyo ndivyo Imani ilivyo. Ni ufunuo wa Mungu. Kanisa limejengwa juu ya mwili ule wote mzima (Mathayo 16:13-19; Wagalatia 1:11-12).

Kuzaliwa upya ni Kristo, ni ufunuo. Mungu amekufunulia siri hii kuu, na hiyo ni kuzaliwa upya. Sasa unakwenda kufanya nini unapokuwa na hilo kundi lote pamoja, ambapoule ufunuo unapatikana kikamilifu, na Mungu akiudhihirisha katika Neno lake kwa matendo yale yale, mambo yale yale aliyotenda, akithibitisha neno? ee, kama kanisa lingejua tu, nafasi yake litajua siku moja. Litakapojua lenyewe ni kitu gani ndipo unyakuo utatokea. Wakati ukaribu. Usisubiri kitambo tena unaona, unajua kuwa kunyakuliwa hakutokei wakati wote? Jambo la kwanza unajua utakuwa umeshapita, mmoja akitoweka hapa na pale. Utatokea jambo la kwanza unajua, na uta.... Hukumu itaipiga dunia. Unasema, “Vema, nilidhani hivi....” “Umechelewa” unakumbuka hawakujua mpaka sikuile walipoingia katika Safina, na ilikuwa wamekwisha chelewa (Matayo 24:37-42). Mwanamwali mpumbavu hakutambua mpaka aliporejea na kugundua mwanamwali mwerevu amekwisha kwenda. Ndiposa alikuwa ameachwa katika kile kipindi cha dhiki kuu. (Mathayo 25:1-13).

Vema, hivyo ndivyo mambo ya Mungu yalivyo. Baada ya kumsadiki, na kumwagalia akitenda mambo mengi mpaka inakuwa kama njia ya kawaida. Na hiyo ndio hali nadhani kanisa litakayo kuwa nayo kabla tu ya kuja kwa Bwana. **Hivyo unyakuo utatokea tuu katika njia ya namna hiyo. Utakuwa tu kwa njia ya kawaida ya kufuata mandiko na mipango ya Mungu.**

Tunahitaji kupokea neema ya kunyakuliwa. Tunataka tuweze, wakati siri hizi za ngurumo zinapotoka, na kanisa linatwaliwa juu, tunahitaji kuwa tayari kulipokea Bwana, tujalie, tujaribu, Bwana, kwa Neno lako, Acha tuzame na kama tukiona tumeshindwa.....

Na unazungumzia juu ya kanisa kuhusu neema ya Unyakuo, **utatokea wakati tunapoweza kuvunja desturi zetu, kusahau mambo yetu yote ya kidhehebu, na kurejea (Ufunuo 10:1-4).** Yeye atamuonyesha Bibi Arusi jinsi ya kujiandaa kwa Imani kuu ya kubadilishwa, sasa, acha tutafute mfano, tumeona nini ngurumo inamaanisha. Hiyo ni kamilifu, tunajua hivyo. Unaona? Ngurumo ilikuwa ni sauti ya Mungu wakati mhuri ilipofunguliwa.

Je ni wakati? Je sirizote zimekwisha? Je zimeshatoa sauti zote? Je hizo ni ngurumo saba zinazotayarisha zito jambo fulani ambalo kundi dogo, ambalo Yeye analikusanya pamoja lipokee Imani ya kunyakuliwa kwenda katika unyakuo wakati yeye atakapo kuja, kwa kuwa tutabadilishwa mara tu hao Malaika watakapokuja; kutoka muda tu wa kufumba nakufumbua, na tutakuwa tumenyakuliwa pamoja na hao ambao wamelala kumlaki Bwana hewani (1 Korintho 15:51-54).

Maombi yangu ni Mungu kama ikiwa hivyo sijui Bwana. Naliambia tu Kanisa ikiwa kama ni hivyo, Bwana andaa mioyo yetu. Tufanye tayari, Bwana, kwasababu hiyo kuu ambayo historia yote ya nyakati, Manabii wote waliopita wamekuwa wakiutazama wakati huo.

Na mwisho wa wakati wa Wapentekoste tunapaswa kurejea, kulingana na Neno la Mungu anavyo tusaidia usiku huu kukuonyesha hapa, kwamba tutapokea mjumbe ambaye atachukuwa miisho hii yote iliyolegea nje pale na kufafanua siri yote ya Mungu kwa unyakuo wa kanisa (Malaki 4:5-6, Ufunuo 10:7).

Na kisha kunakuja siri za ngurumo ambazo hata hazikuandikwa. Hiyo ni kweli na Naamini kwamba kupitia hizi ngurumo saba zitakuwa zikifunuliwa katika siku za mwisho ili kumleta Bibi Arusi pamoja kwa ajili ya Imani ya kunyakuliwa.

Kwa sababu kile tulichonacho sasa, tusingeweza kufanya hivyo, kuna jambo fulani tunalopaswa kulipigia hatua, hatuwezi kuwa na Imani ya kutosha ya uponyaji wa kiungu (ni vigumu). Tunapaswa kuwa na Imani ya kutosha ya kubadilishwa kutoka katika ulimwengu huu na tutatafuta hilo baada ya kitambo kidogo. Bwana akipenda, tutatafuta wapi imeandikwa. Na Baba, mambo mengi sana yangeliweza kusemwa papa hapa, labda kanisa lisingeweza kuelewa. Lakini naona kwamba utawapa kiu, kutamani kwa namna hiyo, Bwana kwamba watakuja na kuona tuko katika wakati wa mwisho, wakati wa wanaanga.

Naomba, Baba, kwamba watakubali si kujaribu kuyahukumu yale waliyokuwa nayo; ni kujaribu tu kuwapa wao Neema zaidi ya unyakuo. Kwa kuwa saa itakuja ambayo tutapaswa kuwa na nguvu ya unyakuo, sio tu kuponya mwili bali kuubadilisha katika muda wa kufumba na kufumbua. Kristo atakuja dhahiri katika miili yao, mpaka anaweza kubadilisha kwa kifo chake kikuu na kile Yeye alichokinaunua. Labda watalitwaa hii leo’ Ishara hiyo ambayo niliizungumzia usiku uliopita, ishikilie hiyo mbele yao na kutembea kupitia huyu mwanao (tujalie, Baba). Ambapo maono, nguvu, na ulimwengu kwa upande mwingine, nguvu, na ulimwengu wa upande mwingine, unafahamika, na O Mungu, kote siri kuu za Mungu zinafunuliwa katika mihuri saba na kufanywa ijulikane kwa watu. Tujalie Baba. Na nautazamia wakati wa kumwagika kwa Roho wa Mungu katika siku hizi za mwisho ambazo sasa tunaishi kwazo, kwa mwagiko lingine la Roho Mtakatifu kanisani kwa ajili ya Imani ya kunyakuliwa, kabla tu haijaja. Na kila kitu kimewekwa moja kwa moja kwa ajili ya jambo hilo. Na ninaamini sasa tuko katika wakati ambao Neno linapaswa kuwa na nafasi ya kwanza. Na naamini kwamba ni saa ya kuweka pembeni kanuni zetu za Imani na mawazo yetu na kurudi kwenye Neno.....

Yeye aliyakusudia mambo haya yawe hivi, na lazima Yeye atume hili. Jambo la kwanza linalokuja wakati anaanza kushuka kutoka Mbinguni. Kuna sauti ya Mwanao (1 Wathesalonike 4:13-18). Ni nini hiyo. Ni ujumbe wa kuwakusanya watu. Ujumbe ukienezwa, ule mkate ulio hai wa uzima ukimleta Bibi Arusi (Yohana 6:51). Sasa “ni wakati wa kutengeneza taa. Amka na utengeneze taa yako.” (Mathayo 25:1-13). Ilikuwa ni wakati gani? Wa saba, sio wa sita, wa saba. Tazama Bwana Arusi yuaja. Amkeni na mazitengeneze taa zenu na walizitengeneza. Wengi wao waliogunduliwa hawakuwa hata na mafuta yoyote katika taa zao unaona? Lakini ni wakati wa kutengeneza taa ni wakati wa malaki 4. Wakati unakuja... Ni Luka 17: Utabiri wote huu ambao unaweza kwa ukamilifu kuwekwa sawa kwa ajili ya siku hii katika maandiko, tunaona ukitokea hapa hapa.

Lakini kitu cha kwanza ni mwaliko na halafu sauti na halafu tarumbeta; Mwaliko ni Mjumbe akiwatayarisha watu... ya pili ni sauti ya ufufuo. Sauti ile ile ambayo sauti kuu katika (Yohana 11:38-44) Iliyo muita Lazaro toka kaburini kukusanya yule Bibi Arusi pamoja, na ndipo ufufuo wa wafu. Unaona kutwaliwa pamoja nayo. Sasa, tazama mambo haya matatu ya kitendeka. Linalofuata ni nini? Ilikuwa parapanda. Sauti ya tatu ni parapanda, ambayo kila mara sikukuu ya kupiga tarumbeta inawaleta watu waende karamuni; na hiyo itakuwa ni karamu ya harusi ya Bibi Arusi ile karamu ya mwanakondo pamoja na Bibi Arusi mawinguni (Matayo 26:26-30) unaona kitu ambacho ni ujumbe wake ukimwita yule Bibi Arusi pamoja. Kitu kinachofuata ni ufufuo wa yule Bibi Arusi aliye lala, yule aliye lala nyuma huko katika zile nyakati zingine (1 Korintho 15:5-58) wao wanatwaliwa pamoja, na parapanda ile, kwa karamu iliyoko katika mbingu... angani. Kwani hilo ndilo jambo litakalo tukia marafiki. Tuko hapa hapa tayari sasa, jambo la pekee, kanisa likisha toka yapasa likae juani kukomaa, ndipo chombo kikuu cha kuvunia kitakuja. Ngano itaunguzwa, mabua yateketezwa bali (ngano)itakusanywa ghalani mwake. (Matato 13:24; 30,36-43).

Oh, kumbuka wakati alipopita chini pale katika nuru kuu, ikasimama nyuma pale kwenye kilindi cha mto, 1933, mwezi wa 6, aliposema kama Yohana mbatizaji alivyotumwa kutangulia kuja kwa kwanza kwa Kristo, na kutuma wewe na ujumbe ulimwenguni kutangulia kuja kwa pili kwa “Kristo” na kupitia ulimwenguni kote limekwenda. Uamsho moto imekuwa ikijengwa kwa miaka 15 na karibu na mlima... Uponyaji wa kiungu kupitia mataifa na nguvu na marejesho... Na sasa, naamini yu tayari kupiga hicho kikomo (kilele) cha kuleta Imani ambayo italinyakuwa kanisa kwenda utukufuni (ni kweli), na amelala katika ujumbe, hakika tuko katika wakati wa mwisho. Tumezungumza juu ya hilo na kila kitu, bali jambo limesogea juu yetu sasa. Ndio, Bwana. Hapa liko moja, hiyo ni kweli.

Kweli naamini, kabla ya kanisa kuwa na unyakuo, linapaswa kuwa na Imani ya kunyakuliwa. Hatuwezi kuwa na Imani ya uponyaji wa Kiungu, achilia peke yake Imani ya unyakuo. Nenda ukapate Imani ambayo itabadilisha na kuhuisha mwili huu, na kutwaliwa. Naamini kuna kanisa katika njia yake usiku huu, nguvu za Mungu aliye hai, ambayo watu watanena Neno hapa na pale, na litamemetesha nuru, na kanisa linatoka, sio msoma mawazo sio mmoja wa hawa aliye vaa, anayefanya kuigiza; bali aliye halisi, kwa kweli, na aliye halisi haswa aliyetiwa mafuta na Roho Mtakatifu, kanisa lililoitwa litoke.

Kila kitu tunachohitaji kwa ajili ya safari yetu hapa duniani: Uponyaji wa kiungu, nguvu za Mungu na vitu hivi vingine viko katika kila mtu binafsi hapa ambaye amepokea ubatizo wa Roho Mtakatifu, kwa kuwa umepandwa katika Kristo. Halleluya. Ubatizo wa Roho Mtakatifu, ndiyo, bwana na kila kitu ulicho kihitaji kwa ajili ya safari ya maisha haya, hata unyakuo uko ndani yako wakati huu usikatae hilo; hiyo ni kweli. Unyakuo uko ndani yetu sasa. Nitalithibitisha hilo kwa injili. Wale aliowaita akawahesabia haki wale aliowahesabia haki akawatukuza, Halleluya. Kisha tuko Mbinguni leo tumetukuzwa katika uwepo wa Mungu sasa hivi (Warumi 8:30).

Musa alikuwa na Neno. Hilo ndilo alilokuwa akihitaji likiwa ni Neno. Hilo ndilo unalohitaji leo. Sio barua ya utambulisho kutoka kanisa fulani. Hauhitaji madhehebu ya kuunge mkono, unahitaji Neno lichukue na unyakuo pamoja nalo. Hauhitaji barua ya utambulisho hauhitaji historia fulani ndefu ya shule fulani ili uponywe asubuhi hii unahitaji kulipokea Neno; hilo litakufanya hivyo.

Bali kanisa la Mungu aliye hai, yeye Bibi Arusi anaendelea tu moja kwa moja namna ile ile. Na atakwenda katika unyakuo kwa Neno litaunganika pamoja. Kama sisi tu sehemu ya Kristo, sehemu Yake, hatuna budi kuwa Neno lake, kwasababu Yeye ni Neno. Hiyo ni kweli. Ndio Bwana.

Kama tujuavyo tu sasa, kama mtu fulani alivyoniuliza muda mchache uliopita juu ya kuja kwa Bwana nakunyakuliwa. Tunajua tumeishi nje ya wakati. Saa ya unyakuo iko mlango. Na tunapotazamia Imani ya kunyakuliwa ambayo inaweza kuyavuta Mekanisa pamoja na kuyapa nguvu ya kimbinguni ambayo itaweza kubadili miili hii ambayo twaishi ndani yake. Tunamwona Mungu ambaye anaweza kuinua waliokufa chini sakafuni, au nje huko Uwanjani na kuwarejesha katika uhai tena, na kumwakilisha yeye mbele zetu. Wakati tunapo mwona Mungu ambaye anaweza kuondoa kabisa kansa ambayo imemla mtu hadi kivuli, na kumwinua kuwa ni mtu mwenye nguvu na afya hilo linapaswa kuwapa watu Imani ya kunyakuliwa, wakati ambapo nuru hiyo ina memeteshwa huko, mawinguni, na parapanda ikilia mwili wa Kristo utakuwa ukikusanyika haraka pamoja, na kubadilishwa kufumba na kufumbua, na kutwaliwa Mbinguni.

Bali ni dhambi ambayo inawakatilia mbali ya vitu hivi ambavyo mlipaswa kuwa navyo. Ni dhambi ambayo inalivika mbali na ile hali ya unyakuo wakati wote. Ni dhambi, sio jengo, sio kanisa, Bali dhambi ambayo iko kanisani.

Inatenda nini katika miili hii yetu inayokufa? Inabadilisha nia zetu, inabadilisha mtazamo wetu. Inaweka Upendo wetu juu ya vitu ambavyo viko juu. {Wakolosai 3:1-4}, na uvutaji sigara, ulevi, kucheza kamari. Mambo uliyokuwa ukitenda yamekufa. Viko chini na umehuishwa, na nguvu hii ya kuhuisha inaleta mwili wako katika hali ya kunyakuliwa tayari.

Je hatuna furaha? Hatuna jambo lolote la kuonea shaka, hakuna chochote. Tumetia nanga katika Kristo, tumekaa katika ulimwengu wa roho, tukinyakuliwa katika neema ya unyakuo sasa hivi, tukikaa katika uwepo wake katika ulimwengu wa kiroho katika Kristo Yesu. {Waefeso 2:6} kifo chenyewe hakiwezi kutugusa: tumetia nanga, hakuna chochote kiwezacho kutusumbua, tumelindwa tu kwa urahisi na tusubiri kuja kwake. Na tunafurahi kwa jambo hilo.

Hiyo ndiyo sababu nina amini ya kwamba wakati Bibi arusi anapoitwa au kuchaguliwa na kuwekwa katika kitabu cha uzima. Kutakuja sauti kutoka mbinguni ambayo itachukua ubatizo wa namna hiyo wa Roho Mtakatifu kwa Bibi Arusi huyo, ambayo itamtwa kutoka katika dunia katika neema ya kunyakuliwa. Mungu aliahidi hilo.

Nukuu Kwa Kiingereza

Yakini 30- December 62 Asubuhi Uk 35 Kiingereza “Yezebeli Aliyejipodaa” Para E –44 “Painted Face Jerebel Para 44”

Israel Katika Kadesh Barnea Para 79.

Tuonyeshe Baba 7 September-1953 A Chicago Para E-85-86.

Kuthibitisha Neno Lake Para 105-106.

Ulimwengu Unamomonyoka Tena 27-11-1963 Para E-7.

Kristo Ni Siri Ya Mungu Iliyofunuliwa Uk 37-38, Mhuri Wa Pasaka Uk 18.

Kung’ang’ania 63-0113e Para E-7.

Kuchagua Bibi Arusi Para 203.

Balm Katika Glead 24-1959 Para E-6

Sikukuu Ya Baragumu Para 270.

jiwe la kiroho la kujengea na 133 kutoka kwenye Neno lililofunuliwa la saa hii, iliyokusanywa na Gerd Rodewald Friedenstr. 69 D – 75328 Schomberg, Germany (+49) 72357613 Fax : (+49) 72353306. www.biblebelievers.de

Anakuja mmoja na ujumbe ambao ni moja kwa moja ni Biblia na kazi ya haraka itaizunguka dunia na mbegu zitaingia magazetini, vitu vya kusomea, mpaka kila mbegu iliyochaguliwa kimbele imesikia. (Ndugu Branham katika mwenendo utaratibu na mafundisho uk 724)

Kwa nakala zaidi: kiingereza, kiswahili, andika kwa:

Charles E. Y. Kanju,

Box 553 Korogwe - Tanga

E-mail: Chaelika@live1.com

Cellphone: 0784 704299/ 0718230098